

Tamathali za Usemi na Taswira katika Utenzi wa *UKIMWI ni Zimwi*

Rayya Timammy
Chuo Kikuu cha Nairobi

Ikisiri

Utenzi wa *UKIMWI ni Zimwi* ni kazi iliyotungwa na Mahmoud Abdulkadir wa Lamu katika mwaka wa 2001. Huu ni utenzi ambao mwandishi aliyutunga kwa lengo la kuwajua watu athari za janga la UKIMWI. Utenzi huu umeandikwa katika lahaja ya Kiamu. Maudhui na dhamira ya kazi ya fasihi haziwezi kuwasilishwa na kuwafikia wasomaji bila ya kuwako kwa lugha. Matumizi ya lugha ni mapana kwani huhusisha tamathali za usemi, uteuzi na mpangilio wa maneno basi, sajili za lugha, matumizi ya nahau na misemo n.k. Katika makala haya, ninashughuliki hasa matumizi ya tamathali za usemi na taswira katika utenzi wa *UKIMWI ni Zimwi*.

Maneno Muhimu: tamathali, usemi, taswira, utenzi

Utangulizi

Utenzi katika fasihi ya Kiswahili umehusishwa kwa kiasi kikubwa na uwasilishaji wa maudhui ya kidini, visa na matendo ya kiajabu na ya kishujaa (angalia utenzi wa Al- Inkishafi, Fumo Liyongo n.k. (Mulokozi, 1989). Kwa maoni ya Miller (1990) na Wamitila (2001), tenzi katika fasihi za Kiafrika na hata fasihi za kilimwengu, huhusika na uwasilishaji wa matendo au visa vya kishujaa vinavyohitaji utambaji mrefu. Tenzi za Kiswahili hali kadhalika zimekuwa zikihusishwa na uwasilishaji wa maudhui ya kifalsafa, dini, wasifu na kwa kiasi, mambo ya kidhahania (Mulokozi 1989, Wamitila 2001). Katika misingi ya kimaudhui haya ndio matarajio ya kila utenzi. Badala ya kukutana na mashujaa na matendo yao ya ajabu au mambo ya dini, Abdulkadir ameamua kuwasilisha na kulishughulikia tatizo la kijamii, UKIMWI ambalo mbali na kutambwa kwa urefu limewasilishwa pia kama ndilo tena mhusika mkuu katika utenzi wote. Kwa kuwa tenzi ni tungo ambazo zinatoa habari kwa urefu na kwa ufasaha basi mtunzi aliona ndio fani ya kutumia kwa kina alichouzungumzia ugonjwa huu na hivyo kuwa na mvuto mkubwa.

Historia Fupi ya Mtunzi wa *UKIMWI ni Zimwi*

Utunzi huu uliandikwa na Mahmoud Ahmed Abdulkadir ambaye alizaliwa tarehe 21 Februari 1952 lakini anatajika kwa lakabu yake ya MAU. Ushairi ni fani ambayo imekuwapo katika familia yake kwani wazazi wake wote wawili walikuwa washairi

kama washairi wengine ambao ushairi uko katika familia zao (Abdulatif Abdalla babu yake alikuwa mshairi; Ahmed Nassir). Mbali na ushairi, Ustadh MAU kama anavyojulikana anafunza madrasa na kutoa khutba miskitini. Amechangia sana katika shughuli za kijamii zinazoathiri jamii ya Lamu. Kwa mfano anajishughulisha katika shughuli za kielimu ikiwa zote za kidini na kidunia. La muhimu zaidi ni kuwa anashughulika sana katika kuendeleza au kuzindua jamii katika maswala tofauti kupitia mashairi yake kama kuzindua jamii kuhusu majukumu yao katika siasa na jamii (angalia utenzi wa Mwangaza wa Siasa, Elimu ya Uraia, Mikhadharati n.k.).

Kazi Zake

Ametunga kazi nyingi sana zikiwepo tungo ndefu au tenzi na pia tungo fupifupi. Miongoni mwa tungo zake fupi anazungumzia maswala kama lugha ya Kiswahili, jahazi ambalo linahusu uchumi, faida na umuhimu wa kusoma na elimu, umuhimu wa vitabu, usafi, kuhimiza watu kusaidiana, ufisadi, magonjwa kama kifua kikuu na UKIMWI, kusifia wanawake, utamaduni wa Mswahili na mengine mengi.

Mbali ya tungo hizi fupi ametunga tungo nyingine ndefu zinazozungumzia maswala tofauti kama wasia kwa wasichana, wasia kwa wanaoana, maswala ya siasa kama wajibu wa raia, uzinduzi wa kisiasa, haki za watoto, mihadharati na janga la UKIMWI. Katika makala haya, tutajikita katika kazi mojawapo ndefu ili kuelezea tamathali na taswira zilizotumika humo.

Utenzi wa UKIMWI ni Zimwi ni utenzi unaozungumzia swala la UKIMWI kwa kina. Mshairi mwenyewe anaeleza kuwa utenzi wake una sehemu sita. Mtunzi ameeleza UKIMWI ni nini na amejaribu kuonyesha chanzo cha ugonjwa huu kiwakati na mahali. Pia ameeleza nadharia kuhusu ugonjwa huu ulivyoibuka na husambazwa vipi; kuu ya sababu hizo akionyesha kuwa ni uzinifu kutokana na mtazamo wake. Mwisho amezungumzia hasara zinazosababishwa na ugonjwa huu mfano ni kama kufa kwa watu wenye utaalumu tofauti. Mtunzi amekazania zaidi sababu hii ya uzinifu hasa kwa kuwa yeye ni shekhe na pia kwa kuwa ameutunga utenzi huu kwa mtazamo wa kidini. Kwa vile alitunga kitambo alionyesha kuwa ugonjwa huu hauna dawa iwapokuwa tunajua kuwa sasa dawa za kupunguza makali ya maradhi haya zipo. Mwandishi anaweza kuwa pia hakuonyesha kuwa dawa zipo pengine kutokana na mtazamo wake. Kwa vile alitunga utenzi huu kwa mtazamo wa kidini na kuonyesha kuwa watu walienda kinyume na maagizo ya kidini ndipo Mungu akaleta adhabu.

UKIMWI ni Zimwi ni utenzi wa Mahmoud Abdulkadir, msomi na mtaalamu wa dini kutoka Lamu. Ametoka mchango mkubwa katika mambo ya kijamii yanayoathiri jamii ya Lamu. Huyu ni mshairi wa Kiswahili anayejitolea na ambaye amefanya mengi katika kuelimisha kuhusu UKIMWI Lamu. Utenzi wa *UKIMWI ni Zimwi* una beti 289 na ulitungwa na mwandishi kwa madhumuni ya kuelimisha wanajamii kuhusu baa hili katika mwaka 2001. Una muundo wa mishororo minne

katika kila ubeti na umedumisha bahari moja kutoka mwanzo hadi mwisho. Katika kipengee hiki, utenzi huu umeakisi sifa za kimsingi za tenzi za Kiswahili. Lakini katika kipengee cha maudhui na wahusika, utenzi huu umechukua mwelekeo tofauti kabisa. Ukiukaji wa kaida hizi za matarajio ni jambo tunalotaka kulifuatilia hapa kwa sababu linaonekana kwamba haya ni mageuzi ya maksudi. Kupitia kwa utenzi huu, ninadai kwamba tamathali za usemi na taswira alizotumia ni mambo yanayochochewa na kuhusiana moja kwa moja na mada anayoizungumzia.

Kwa kawaida suala hili la UKIMWI huelezwa zaidi kwa kutumia fani ya drama/tamthilia zinazoigizwa na makundi kuelimisha jamii. Lakini msanii anaonyesha kuwa hakungojea makundi hayo yaelimishe jamii bali aliona ni jukumu na nafasi yake kuelekeza. Mtunzi huyu anatumia shairi hasa kwa kuwa anatokea eneo ambalo limekuwa ndilo chimbuko la ushairi Afrika Mashariki na lilikuwa na tarehe ndefu ya ushairi na kuna washairi wengi waliotoka eneo la Lamu. Vile vile ushairi ndiyo fani muafaka kwa kuwa mpaka wa leo hakuna makundi yanayotumia maigizo katika eneo hilo na pia kutokea miaka ya nyuma (1980). Mahmoud Abdulkadir alikiri kuwa mashairi yana nafasi muhimu katika kueleza watu fikra na mawazo na hasa eneo la pwani. Kulingana naye anaona kuwa watu wameutambua zaidi ujumbe wa mashairi kwa sababu ya mdundo na mnato wa maneno yake. Maoni haya yake pia yameungwa mkono na Chiraghdin katika utangulizi wa Sauti ya Dhiki (1973) anapokiri kuwa kwa Waswahili njia nzuri ya kueleza alilionalo moyoni ni kwa kutunga mashairi. Mtunzi wa UKIMWI ni Zimwi anatwambia:

Nami hulifanya hili
Kwa ajili ya mawili
La kwanda ni waswahili
Nataka kukhubiria

Nayo ya pili sababu
Haya mimi kukutubu
Naamini ni wajibu
Mola amenifaradhiya
(beti 7-8)

Hivyo, anataka kueleza jamii na hili analiona ni jambo ambalo lazima alifanye kulingana na dini. Kwa kutumia tamathali za usemi na taswira, msanii anafaulu kutekeleza lengo lake kwa kiwango kikubwa. Tamathali za Usemi huwa ni ukiushi wa matumizi ya lugha unaofanywa kimaksudi katika kipengele cha maana na mpangilio wa maneno ili kupatikane maana mpya au kwa lengo la kusisitiza (Mulokozi na Kahigi, 1979; Mbatia, 2001). Tamathali za usemi ni nyingi sana kwa mfano tashibihi, sitiari, tasifida, tashihisi, chuku, kinaya, dhihaka, maswali ya balagha na tabaini. Katika kazi hii mwandishi ametumia tamathali za usemi kadhaa kwa mfano sitiari, tashibihi, tabaini, tashihisi, maswali ya balagha, miongoni mwa nyingine. Zaidi tutaangalia hasa sitiari na tashibihi kwa sababu hizi hutumika hasa katika kuundia taswira na kwa jumla sitiari huleta udhahiri na msisitizo katika

maelezo. Mbali ya kuzitambua tamathali hizi, tumeonyesha mchango wake katika kuyawasilisha maudhui na mawazo ya mwandishi. Hivyo katika makala haya, tunaangalia vipi tamathali hizi zinapotumiwa katika kuchora picha halisi huweza kuwa silaha ya kuamsha na kuhamasisha wanajamii kujiepusha na janga hili.

Tamathali za usemi na taswira zilizomo katika utenzi huu zinaweza kugawanywa kulingana na vipengee sita vilivyoshughulikiwa katika utenzi. Taswira haswa ni utumizi wa lugha inayojenga picha akilini mwa msomaji ambayo huibua hisia fulani kwa msomaji (Mohamed, 1995; Wamitila, 2003).

Mtunzi ametumia tamathali za usemi na taswira katika sehemu ya kufafanua UKIMWI unavyoambukizwa na madhara yake. Tokea mwanzo, msomaji anaomba msamaha kwa kuyazungumzia maswala haya waziwazi; ijapokuwa anakiri kuwa mengine amefumba na ndipo anapotumia tamathali za usemi na taswira.

Samahani wasikizi
Kutaya mengine wazi
Hayo kufumba siwezi
Lengo halitotimiya (ub.128)

Ni lazima kutobowa
Waziwazi kufunuwa
Ili tupate elewa
Sute tutaosikiya (ub.129)

Hayatoshi ya mafumbo
Kuweleza hili yambo
Hizi si za kwimba nyimbo
Bali ni masomo haya (ub.130)

Tunaona tabaini ya kwanza hapa juu “hizi si za kwimba nyimbo” ikitumika kusisitiza kuwa haya anayoyasema si mambo ya mchezo si ya kusema tu bali ni mambo muhimu sana.

Tamathali za Usemi na Taswira za Kufafanua UKIMWI

Tukianza tunaona kuwa mtunzi ametumia tamathali ya aina ya sitiari katika jina la utenzi wenyewe. Ni sitiari inayolinganisha UKIMWI na zimwi, “UKIMWI ni Zimwi”. Ulinganishi huu wa moja kwa moja ni taswira inayoakisi kabisa ukweli wa ugonjwa huu. Hii ni taswira kuu ambapo sitiari na taswira hii inatawala na kuchukua nafasi kuu katika utenzi wote. Taswira hii ina uhusiano mkubwa na maudhui ambayo ni swala la UKIMWI ambalo ni muhimu wakati huu. Zimwi ni kiumbe kipatikanacho katika hadithi za fasihi simulizi za Waswahili ambacho huogofya na kinameza na kumaliza binadamu. UKIMWI unalinganishwa nalo kwa vile unavyoangamiza watu wengi. Sitiari hii inatumika tena katika ubeti wa 3,

UKIMWI tuangamize
Au na tuupunguze
Ili usitumalize
Ni zimwi hutubugiya

Msomaji anaposikia jina la ‘zimwi’ anakumbuka zile hadithi za fasihi simulizi na jinsi zimwi katika hadithi husika linavyochorwa kuwa ni kiumbe kinachodhuru watu, hivyo sitiari hii inakuwa muafaka sana. Hii pia, tunaweza kusema kuwa, ni taswira ya kimsingi kwa vile inachukuwa nafasi kubwa katika muundo wa utenzi kwani mbali ya kuchukuwa nafasi hii pia inaelekea kuitawala kazi hii. Sitiari hii imeendelezwa katika beti nyingine na ni kama uzi unaoshikilia utenzi mzima (angalia beti 157, 159 na 163).

Katika ubeti wa 18 mtunzi anatuchorea taswira ya maono anapolinganisha virusi vya UKIMWI vinavyoungia mwili wa binadamu na jinsi mchwa wanavyoingilia mti na kuuharibu ukamumunyuka. Hii ni sawa na viini vya UKIMWI vinapomuingia binadamu na kuupujua mwili wake hadi akamalizika. Picha hii inaakisi vizuri kwa vile mchwa huingilia mti bila hata mti huo kwa nje kuonyesha athari mpaka muda mrefu baadaye kama ulivyo ugonjwa wa UKIMWI.

Cha tano namna gani
Hupenyeza muwilini
Ngaliya mtwa mtini
Mtu unapomngiya (ub. 18)

Mbali na kuwa ni taswira ubeti huu pia ni tashibihi. Neno ‘ngaliya limetumika kumithilisha katika muktadha lilipotumika katika lahaja ya Kiamu. Hivyo tashibihi hii imetumika kulinganisha UKIMWI unavyoudhoofisha mwili wa binadamu sawa na mchwa wanavyouharibu mti.

Mtunzi anatomia sitiari nyingine katika ubeti wa 23 kufananisha kinga za mwili na askari.

Ndizo kinga ya muili
Ni askari kamili
Na kabisa hakubali
Adui ndani kungiya (ub.23)

Kwa vile askari haruhusu adui kuingia nchini au ndio wanaolinda nchi kutokana na kuvamiwa na maadui, nazo kinga za mwili haziruhusu maradhi kuingia muilini. Mbali ya kuwa ni sitiari inatupa taswira ya hao askari wanavyofanya kazi. Taswira hii ya vita na askari inaendelezwa na mtunzi katika ubeti 32 anapotoa mfano mwengine wa ulinganishi wa askari na kazi ya kulinda. Anaonyesha jinsi mtu yupo kwenye mji ambao umevamiwa na maadui, na hakuna jeshi (askari) la mji huo la kutoa ulinzi, basi wananyang’anyia kuvamia bila upinzani wowote.

Mfanowe wewe hapo
Ni maadui wapapo
Mui jeshi halipo
Ni kinyang’anyiro hoyo (ub. 32)

Katika ubeti wa 37 anatumia tashibihii anapoufananisha UKIMWI na ndimwi ambayo inakupa picha ya hao minyoo.

Na hunu ndiwo UKIMWI
Nimeupa ina zimwi
Hubugiya kama ndimwi
Kipitacho huchakiya

“Ndimwi” ni neno katika lahaja ya Kiamu lenye maana ya “minyoo” walioko chonjo kula chochote kinachoingia katika tumbo la binadamu.

Katika ubeti wa 41 na 42 mtunzi anatumia uhuishi anapoupa ugonjwa huu sifa za kibinadamu anaposema kuwa unatafuna. Pia katika ubeti huo wa 42 mwandishi anatumia taswira ya maono kutuonyesha jinsi zimwi linavyomaliza watu au namna UKIMWI unavyofanya kazi kwa kasi kumaliza watu. Yaani, kwanza tunaonyeshwa jinsi (ugonjwa) zimwi lilikuwa likichukuwa muda kuua watu lakini sasa linachukuwa watu kwa kasi kwani “linamiza” badili ya kutafuna.

Kwanda lalikitafuna
Na sasa meno halina
Na muda piya hapana
Humiza moya kwa moya (ub. 42)

Tamathali za Usemi na Taswira za Namna Unavyoambukizwa

Mtunzi anapoeleza chanzo cha ugonjwa huu anatuchorea picha ya kutuonyesha maradhi yalianza katika makundi ya watu waliokuwa wamejiingiza katika machafu ya kila aina. Hivyo msomaji anafanywa atafakari akilini (ub. 85- 106).

Ni kutokana na dini ya Kiislamu ndipo anapotupatia taswira nyingi sana. Ijapokuwa tumesema tenzi nyingi za awali zilikuwa za kidini, utenzi huu haupo katika tapo hilo. Hata hivyo msanii anatutolea taswira kutokana na dini ili kufafanua zaidi swala lake la UKIMWI kwani anachukulia kuwa njia kuu ya kueneza ugonjwa huu ni kwa njia ya zinaa kwa vile dini ya Kiislamu inapinga jambo hilo mtunzi anatutolea mifano mingi ya watu walioangamia. Katika ubeti wa 64,

Mfano kuna tufani
Kuna kiswa cha Karuni
Kadhalika Firauni
Na manginge imetaya (ub. 64)

Mtunzi anatoa visa vya watu mbalimbali walioangamia kutokana na maovu (ub 64-67). Anatoa mfano au taswira ya Karuni na Firauni, kaumu ya Adi na Thamudi na mwisho, watu wa Lutwi (wenyeji wa Sodom). Ijapokuwa haelezi yote yaliyotokea katika jamii hizi mbalimbali, lakini kwa anayeifahamu dini, picha inamjia akilini ya maangamizi. Na kwa kuwa alitueleza anawaandikia Waswahili walio Waislamu bila shaka wanafahamu visa hivi vilivyoelezwa katika Quran (angalia kuhusu kaumu au watu wa Lut katika sura Al A’raf:80-84, sura Hud:77-83; watu wa Ad katika sura Al A’raf: 65-72, sura Hud: 25-38,50-60; watu wa Thamud

katika sura Al' Araf: 33-79, sura Hud aya 61-68). Tazama beti hizi mbili zinazofuata.

Kuna na kaumu Adi
Wako na hao Thamudi
Kwa maovu kushitadi
Hawa waliangamiya (ub. 65)

Hao mbwa Lutwi kaumu
Kiswa chao maalumu
Mui wao ni Sodumu
Zitabu zote hutaya (ub. 67)

Katika ubeti wa 75 na 76 mwandishi anatumia sitiari nyingine anapoonyesha jinsi watu wa Lutwi walivyowakataa wanawake na badili yake wakaingilia mambo ya uhanithi. Mtunzi anaona uhanithi ni sababu mojawapo ya kuzuka kwa maradhi ya UKIMWI kama laana kutoka kwa Muumba (angalia ubeti wa 85 hapo chini).

Kamba zetu ni donasi
Sambusa si zetu sisi
Hutuembeza upesi
Hushibisha mara moya (ub. 75)

Sambusa kwetu sitamu
Zimezidiwa na ndimu
Wala hatwisi hamumu
Zikiketi huregeya (ub. 76)

Mungu huweteya rada
Kwa maradhi yaso ada
Wala kwa wao jududa
Kattu hayakutokeya (ub. 85)

Ile dhana ya tundu ya nyuma ya binadamu inalinganishwa na donasi, aina ya chakula cha mviringo, na uchi wa wanawake kulinganishwa na sambusa yenye pembe tatu. Hivyo anazungumzia suala nyeti kwa njia ya kufumba kwa kutumia hizi sitiari kwani ni mambo yasiozungumzwa waziwazi. Mshairi aliweza kuzungumzia swala la watu wa Lut kujamiiana wanaume kwa wanaume na kuwakataa wanawake. Msanii anafaulu sana kwani picha au taswira za vyakula hivi zinafahamika sana. Mshairi anaonyesha jinsi wanaume walianza kujamiiana wenyewe kwa wenyewe na halikuwa la ajabu tena wakiwaacha wanawake ambayo ni kaida. Pia anaonyesha jinsi wanawake nao walianza usago.

Kwa wanawake usago
Kwa wanaume zishogo
Kugagunana sibago
Yamekuwa mazoweya (ub. 91)

Mwandishi anatoa taswira nyingine katika ubeti wa 121 akizungumzia jinsi UKIMWI unavyosambazwa. Ile njia kuu ni ya kupitia ngono. Taswira aliyoitumia hapa inakuwa muafaka kwani ameweza kuzungumzia mambo yasiyozungumzwa hadharani kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja.

Waama kutiya kingi
Kwa la keramu viringi
Siulize mambo mengi
Kheri andika wasiya (ub. 121)

Mwandishi amefaulu kutumia sitiari hii ya mchezo wa keramu kwani ni mchezo unaofahamika sana miongoni mwa Waswahili. Na kule kutia vidubwasha vya mchezo huu katika zile tundu, kumefananishwa na kujamiiana.

Katika ubeti wa 123 anaonyesha jinsi mtu mwenye UKIMWI hatarajiwi kufanya kazi kutafuta riziki kwani huwa anasubiri mauti tu.

Nikusuburi wakati
Yarezareza mauti
Na mtu simlaiti
Wali kwenda kuzengea (ub. 123)

Neno ‘wali’ ni ishara ya kufanya kutafuta riziki kwa kufanya kazi.

Wazo la kuwa UKIMWI husambazwa kwa kujamiiana linasisitizwa sana mtunzi anaposema:

Donasi au sambusa
Ukidara umekwisa
Litalosaliya sasa
Ni wakati kungojeya (ub.122)

Donasi zimetumika kusimamia kujamiiana kwa njia ya nyuma kwa wanaume na sambusa zimetumika kusimamia sehemu za siri za wanawake. Katika ubeti wa 125 mtunzi anasema ikiwa kati ya mke na mume, mmoja ni asherati atamletea mwenzake balaa hiyo.

Hata kwa ngono halali
Kiwa katika wawili
Mmoya ni baradhuli
Mwendiwe atamtiya (ubeti 125)

Ubeti wa 126 anamlinganisha mwanamume na kidume (mwanamume anayejifanya ni mume sana), na atuonyesha kuwa huyu anaona ni lazima ‘akageme mnazi’ anasema:

Baina mke na mume
Mume kiwa ni kidume
Sharuti nde kageme
Na mke tampekeya (ubeti 126)

Yaani mtu huyu anajifanya ni mume lazima akazurure nje kutafuta wanawake. Na huku kuzurura na wanawake tofauti ndiko kunakosababisha kuenea kwa ugonjwa huu wa UKIMWI.

Tamathali za Usemi na Taswira Kutokana na Madhara

Hasara za janga hili zimeenea kote duniani na hazihesabiki. Anapoanza kuzungumzia hasara za ugonjwa huu anatumia sitiari na analinganisha uzito wa hasara ya janga hili katika ulimwengu wote na uzito wa majabali.

Hasara za kwelikweli
Uzito wa majabali
Umetiya janga hili
Kote katika dunia (ub.148)

Hii inakupa picha ya jinsi ugonjwa huu ulivyo thakili kwa mwenye kumshika na anayeuguza. Kwa kiasi kikubwa ufundi wa utenzi huu watukumbusha ufundi aliotumia Seyyid Ali bin Nassir katika Al-Inkishafi. Kama Inkishafi, msanii anachota toka katika mazingira ya pwani alimoinukia.

Swali la balagha limetumika katika ubeti wa 156. Mtunzi anazungumzia jinsi walimu wengi walivyofariki kutokana na ugonjwa huu na anatumia swali hili la balagha kuonyesha kuwa ikiwa ilimu itaharibika basi mambo mengi au yote yataathirika.

Walimu wakiondoka
Mambo hukharabatika
Ilimu kiporomoka
Lipi litalosaliya? (ub.156)

Ugonjwa huu wa UKIMWI katika utenzi huu wa *UKIMWI ni Zimwi* kwa kijumla umepewa sifa za binadamu au umehuishwa kwa kulinganishwa na zimwi na tunaona tashihisi nyingine katika ubeti huu asemapo:

Hungiya pasi na hodi
Tena hupenda zaidi
Zituo za ufisadi
Hoko ndiko huguriya (ub.161)

Mtunzi ametumia uhuishaji huo kuonyesha kuwa UKIMWI unapatikana sana katika kumbi za burudani kwani ndiko unakopenda kuishi.

Katika ubeti wa 162 msanii anatuchorea taswira inayotokana na sitiari anapofananisha mahali ambapo UKIMWI unapatikana kwa wingi na jinsi kumbi kumbi wanavyojiingiza katika moto wanapovutiwa na ule mwanga.

Henda likapija kambi
Kwenye za fisadi kumbi
Angaliya kumbikumbi
Motoni kuyatiliya (ub.162)

Ingawa moto ni hatari kwa maisha yao, kumbikumbi wanajiingiza katika moto na ndivyo watu wafanyavyo kwa vile japo wanajua kuna hatari ya UKIMWI lakini wanapenda kwenda kwenye maeneo ambayo ufisadi hutendeka. Katika sehemu hizo ndio wanaupata ugonjwa huu.

Katika ubeti wa 167 anauliza swali lingine la balagha “ni nyani tafanya kazi?” kwa sababu kila mtu ni mgonjwa, hakuna wa kufanya kazi.

Ni nyani tafanya kazi?
Watu wote hawawezi
Wazawao siku hizi
Ni lini kuinukiya

Mwandishi ametumia taswira katika ubeti wa 170 kuonyesha kwamba hata kama binadamu wengine wanazaliwa kwa wingi, lakini inachukuwa muda kukua. Hivyo kutakuwa na hasara kutokana na watu wanaokufa kwa UKIMWI.

Tabaini imetumika anaposema ‘mwanadamu si kuku’ kwa lengo la kuonyesha makuzi ya binadamu ni tofauti na wanyama wengine.

Hata kama kula siku
Huzaliwa malukuku
Mwanadamu si kuku
Kishopoka hukimbiya (ub.170)

Watoto kwa kawaida huchukua muda kukua na hata kuweza kushika madaraka yanayoshikwa na watu wazima. Kwa kuwa watu wanakufa kwa UKIMWI, kutakuwa na ombwe tupu ambapo kutakuwa hakuna watu wa kufanya kazi mbalimbali. UKIMWI pia unalinganishwa na mzigo mzito kwa wale watoto wanaobaki bila wazazi.

UKIMWI ni zigo zito
Kwa hawa wengi watoto
Wachandama mkokoto
Wazazi kitanguliya (ub. 173)

Dhana hii ya hasara ya UKIMWI imesisitizwa sana hasa msanii anapotueleza tena kuhusu ‘zigo zito’ katika beti 175-176 anaposema:

Hongeya yao idadi
Kula kuchapo huzidi
Na nti nyuma hurudi
Kwa mzigo kutwemeya

Umetwemeya mzigo
Metuzamisha kishogo
Kali mno hili pigo
Mungu amezotweteya (b.175-176)

Hii pia ni taswira tunapochorewa picha ya mtu aliyebeba mzigo ambao ni mzito hadi amepeta kishogo. Taswira hii imeunganishwa na sitiari inayoonyesha kuwa UKIMWI ni adhabu ya Mungu.

Katika ubeti wa 177 mtunzi anaendelea kuonyesha hasara ya UKIMWI na anatumia jinsi katika baadhi ya mitaa kuna majumba lakini hakuna watu wa kukalia nyumba hizo. Picha au taswira hii ni ya kimaielezo ambayo haina maana iliyofichika; inatuonyesha tu hasara ya kiuchumi, na picha ya kifikiria kuona jinsi nyumba zinatafuta wapangaji. Hapa tena tunakumbuka Al inkishafi tulipochorewa yale magofu na mahame ya mji wa Pate katika karne ya 18. Mwandishi anaonyesha upeo wa namna watu wanavyodhalilika mpaka wako tayari kumhonga Izraili malaika wa kutoa roho.

Kumhonga hawaizi
Ili washushe pumzi
Izraili hawezi
Hongo kwao kupokeya (ub.177)

Picha ya mtu anayetaka kufa inakujia machoni. Kwa kawaida tunachukulia kuwa watu huwa tayari kumhonga Izraili, ambaye ni malaika wa kuchukuwa roho, asiachukue maisha (uhai) yao. Lakini hapa tunachorewa picha ya kinyume cha matarajio ambapo mgonjwa wa UKIMWI yuko tayari kufa.

Mtunzi anapoanzia kuzungumzia dawa ya janga hili, anatuonyesha kuwa bado haijavumbuliwa. Katika ubeti wa 186 anatumia tashibihii kuonyesha kuwa Wazungu wamejaribu jitihada zote lakini hawajafaulu kupata dawa hiyo ya kutibu ugonjwa wa UKIMWI.

Hao walo walimwengu
Wasifikao wazungu
Hupaa kama zipungu
Na bahari kuzamiya (ub. 176)

Wazungu wanaoongoza kwenye sayansi ya tiba, wanalinganishwa na aina ya ndege aitwaye ‘kipungu’ kwani anaweza kupaa juu sana na ana uwezo wa kuranda kote. Hivyo kule kupaa kwake kumelinganishwa na jitihada kuu za wazungu kuyatafutia tiba maradhi haya bila kufaulu. Hili linaafikiana vizuri na methali ya Kiswahili isemayo “ angeenda juu kipungu haifikii mbingu” kuwa hata wangafanya juhudi za aina gani kupata tiba maadamu ni jambo Mungu haliafiki basi hawatafaulu.

Mwandishi analinganisha virusi vya UKIMWI na ‘tunu’ ambayo pia ni kinaya cha hali ya juu, kwani tunu anayotunukiwa mtu kawaida inafaa iwe kitu kizuri na sio virusi vya magonjwa.

Kiishi muda mrefu
Mwenye nazo huswarifu
Kawatiya maalifu
Tunu kiwatunukiya (ub. 195)

Mwandishi anamfananisha mgonjwa wa UKIMWI aliye na hasira na chuki na anayepita akiusambaza ugonjwa huu sawa na mtu mwenye wazimu aliye na chupa ya sumu anayepita akitia sumu hiyo kwenye chakula kinacholiwa na watu wengi. Taswira hii ni mjarabu sana kwani unapopata virusi hivyo ni sawa na kula sumu kwani mwishowe ni mbaya (ubeti 196-197).

Wala haiwi ni haki
Kumuwata makhluki
Mwenye hasira na chuki
Wende utwa kuwatiya (ub. 196)

Mfano mwanda wazimu
Alo na tupa ya sumu
Hupita kwenye kaumu
Chakula kunyunyiziya (ub. 197)

Hii pia ni sitiari ambapo virusi hivi vinaambiwa ni sumu.

Nataraji mefhamu
Virusi hizi za sumu
Humpasa mwanadamu
Aso nazo kamngiya (ub. 115)

Virusi hivi vinapomuingia mtu huwa ni kufa tu kama vile sumu inavyoua kulingana na maelezo ya mtunzi. Kwa wakati wa sasa kama tulivyotaja awali kutokana na maendeleo ya kiutabibu dawa zipo za kupunguza makali ya ugonjwa huu au kuuzuia ili mtu aweze kuishi maisha ya kawaida ingawaje ana virusi lakini havionekani kabisa. Lakini kama nilivyogusia mtunzi ni mwalimu wa kidini pengine ameacha kuelezea hayo kimaksudi ili kuwatia waumini hofu ya kutokuwa waasherati kwani hilo ni kosa kubwa kulingana na dini ya Kiislamu.

Anatuchorea taswira nyingine ya mfalme Nimrod (ub. 203-204) aliyesumbuliwa na mbu hadi akajigonga kichwa na kufariki. Msanii anaitumia taswira hii kutuonyesha kuwa kungevumbuliwa dawa za kupunguza nguvu za virusi vya UKIMWI, ugonjwa bado utasumbua hadi watu waache uzinifu na maasi kwa Mungu. Tunajua kuwa dawa zipo wakati huu lakini mtunzi bado anakazania mtazamo wa kidini kuwa ugonjwa huu umesababishwa na kutofuata maagizo ya Mwenyezi Mungu.

Tukumbuke Namrudhi
Mfalume mwenye hadhi
Ni mbu alomuudhi
Hata mauti yakaya (ub.203)

Ni mbu alomshinda
Hata kitwa kakivunda
Nasi tutauma zanda
Nyuma tukitorejeya (ub.204)

Katika ubeti wa 209 mwandishi analinganisha UKIMWI na bomu. Taswira hii ni wazi kabisa na ina nguvu sana maana anataka kuonyesha kuwa kondomu haitoweza kuzuia ugonjwa huu na hata ukivaa ya chuma. Kama tulivyotangulia kusema mtunzi ni shekhe kwa hivyo japo anajua kuwa dawa zimevumbuliwa anajaribu kuonyesha kuwa ugonjwa huu utawacha kusumbua tu pale watu watawacha kuwa wazinifu kwani kulingana na dini ya Kiislamu mahusiano nje ya ndoa ni uzinifu. Kwa kuwa anachukulia mtazamo kuwa ugonjwa huu ni adhabu kutoka kwa Mungu, anaonyesha kuwa hata mtu akitumia kitu gani, bado akiwa hafuati mwenendo anaotaka Mwenyezi Mungu, adhabu itamfikia. Anatomia pia tabaini anaposema ‘licha ya kuwa si nyumu’ kusisitiza kuwa hiyo kondomu yenyewe hata si ngumu vile ilivyo na hivyo haiwezi kuzuia maambukizi.

Haiziwi kondomu
Asilani hilo bomu
Licha ya kuwa si nyumu
Na ya chuma ungetiwa (ub.209)

Bado akiendelea na mawazo hayo hayo, katika ubeti wa 210 anaufananisha UKIMWI na mwamba unaovunja.

Kondomu hukinga mimba
Wala haikingi mwamba
Virusi ambazo kwamba
Ni sugu kupindukiya (ub.210)

Picha hii ina taathira kubwa sana kwani mwamba huweza kuvunja meli kubwa baharini. Kwa kulinganisha virusi vya UKIMWI na mwamba, msanii anataka kutuonyesha ukubwa wa hasara inayoweza kusababishwa na virusi hivi. Hata hivyo imethibitishwa kondomu inakinga ikitumiwa vilivyo.

Mwandishi anatuonyesha kuwa njia ya kipekee ya kuuzuia ugonjwa huu ni kuwa ushikwapo shikamana (ubeti wa 217) kumaanisha kuwa mtiifu na mkweli katika ndoa. Anatomia sitiari kumkanya binadamu asiwe popo kurukia kila mti. Hii ni sitiari muhimu inayomuasa na tabia ya kutanga tanga au kuwa na mahusiano nje ya ndoa.

Kinga kuu iliyopo
Shikamana ushikwapo
Siwe mfano wa popo
Kula mti kuukiya (ub. 217)

Katika ubeti wa 220 mshairi anatomia msemu kumkanya binadamu mwenye tabia hii ya kupenda kuwa na wanawake tofauti tofauti. Tabaini imetumiwa

kuonyesha kuwa hiyo tabia ya ‘kinuka mto’ yaani kubadilishabadilisha wanawake, shida zake ni kubwa mno.

Kazi ya kunuka mto
Balaya zake si toto
Siupuze hunu mwito
Jaribu kuutumiya (ub. 220)

Matamaniao ya ngono au ya kufanya mapenzi yamelinganishwa na maji ya mto yachanganyikayo na maji ya mvua na yanayoshuka kwa kasi kwenye mto unaofurika mpaka ukavunja kingo. Katika ubeti wa 221 mwandishi anatuchorea taswira kwa kutumia tashibihii kufananisha matamaniao hayo na hali hiyo.

Matamaniwa ya ngono
Yana kasi kuu mno
Takupa wake mfano
Ngaliya zimba likiya (ub. 221)

Katika ubeti wa 226 mwandishi analinganisha kuzini na magendo. Ulinganisho huu unaonyesha kwa uwazi jinsi dhambi hii ya kuzini ilivyo mbaya. Kwa vile ubaya wa magendo unajulikana sana, hivyo kwa kutumia ulinganishi huu athari ya ila au tatizo hili inajitokeza zaidi.

Kwangaliya ndicho chando
Kutenda hayo magendo
Hutoweza kuwa kando
Mato yakitanguliya (ub. 226)

Mwandishi anaonyesha jinsi mtu anaweza kuchukuwa muda hata inapojulikana kuwa anao UKIMWI. Hivyo katika ubeti wa 237 anaonyesha vile mwanamke anaweza kuonekana mrembo na asiye na kasoro lakini kumbe ni mtego, ukimkaribia, unapata ugonjwa huu. Ametumia tashibihii anapomlinganisha mwanamke na ulimbo na pia unapata taswira ya mwanamke mrembo.

Tena toto la urembo
Haonekani na kombo
Lakini kama ulimbo
Ukidara meumiya (ub. 237)

Katika ubeti wa 239 msanii ametumia tashibihii na sitiari pamoja kuonyesha na kusesitiza kuwa unaweza kuona mtu anayekuvutia na kumbe ni hatari. Anatuchorea picha ya mwanamke mrembo ambaye ameumbika sihaba na aliyejaza na kumbe ni akhasi. Mwanamke huyu analinganishwa moja kwa moja na aina ya pilipili (hoho) ambazo zinawasha sana. Hapa anamaanisha kuwa ingawa anaonekana kuwa ni mrembo kumbe ni hatari kwa maisha.

Kiliyona toto shoo
Mafuta kama kondoo
Sikaribiye nihoo
Uchenda takuwatiya (ub. 239)

Hivyo usivutiwe na mtu aliyenawiri ukadhania hana huo ugonjwa. Jambo hili mwandishi analikariri sana hivi kwamba katika ubeti wa 240 anasema:

Sikuhadae urembo
Kanena nacho ni chombo
Urembo kwake ni chambo
Cha watu kuhadaliya (ub. 240)

Hapa anatumia sitiari mbili anapolinganisha mwanamke na chombo, na urembo wake ni chambo, yaani mtego wa kuvutia waume. Kumetumika taswira ya uvuvi ambapo chombo mara nyingi hurejelea chombo cha baharini, na kama mvuvi hutumia chambo kumnasa samaki, naye mwanamke hutumia urembo huo kama chambo kuvutia wanaume. Taswira ya uvuvi inaendelezwa tena katika ubeti ufuatao anapoeleza:

Sighurike kwa usemi
Na wake tamu ulimi
Ukanena wangu nami
Mshipi taatiliya (ub. 241)

Msanii pia anatumia sitiari anapoonyesha huo ulimi ni tamu kumaanisha ni wa kutoa maneno mazuri, ya kupendeza na kulaghai. Hivyo basi anaonyesha vile mtu hapaswi kudanganyika na maneno matamu mpaka akavutika. Taswira ya uvuvi inaendelezwa anapotumia neno ‘mshipi’ kumaanisha kumvuta huyo mwanamume kwa maneno ya kuvutia na kupendeza.

Mwandishi sio kuwa anaonya tu wanaume dhidi ya wanawake bali pia wanawake dhidi ya waume. Katika ubeti wa 243 na kuendelea, anamueleza huyo mwanamke juu ya mwanamume ambaye anaonekana ni dume na kumbe ana UKIMWI. Anatumia tashbihi kadhaa kama:

Shungi kama la ekita
Nyeeze humetameta
Rihi njema ya mafuta
Kikupita hukwatiya (ub. 245)

Una jimo kama tiga
Achenda huititiga
Mapesa yeye humwaga
Hajali kuyatezeya (ub. 247)

Tashbihi hizi zimetumiwa kuchora taswira ya maono ambapo tunamuona huyo mwanamume mwenye nywele kama za ‘ekta’ (actor) na ambaye ni mrefu. Taswira hii ni muafaka sana kwani katika jamii ya Lamu, tabia ya kutazama filamu za Kihindi ni kawaida ambapo yule mhusika mkuu ndiye vijana hujaribu kumuiga. Mtunzi anamsifu kuwa ni mrefu kama twiga. Anapomfananisha mwanamume huyo na ‘ekta’, anatahadharisha wanawake wasidanganywe na wanaume wa aina hiyo. Hivyo, ingawa anampatia sifa zote nzuri lakini mwandishi anatutadharisha dhidi

yake kwani huenda ana UKIMWI! Jambo analoonyesha msanii ni kuwa mwenye UKIMWI huwa hana alama ila pale tu ugonjwa unapokuwa wa siku nyingi.

Katika ubeti wa 253 mwandishi anaonyesha kuwa wakati alama zinajitokeza, ufahamu kuwa sasa mtu huyu huwa anakaribia mwisho wake. Kwa sasa hizi dalili hata zinaweza kuwa zisionekane kwani kutokana na tafiti za kimatibabu, kuna dawa zilizovumbuliwa ambazo mgonjwa wa UKIMWI anaweza kutumia na hivyo asionyeshe dalili zinazozungumziwa katika utenzi huu. Tukumbuke utenzi huu uliandikwa zamani kidogo na pia kutokana na mtazamo wa mtunzi, mtazamo wa kidini, ni kama njia ya kuwaogopesha watakaousoma au kuusikiliza.

Umuonapo mekonda
Hata kumshinda ng'onda
Sidhani kuwa humwanda
Huwa kingi ametiya (ub. 253)

Umuonapo hupepa
Maguu chenda hutupa
Yuwa amevunda tupa
Mwana mbwa kumpokeya (ub. 254)

Mwandishi hapa anatuchorea taswira za jinsi mwathiriwa wa UKIMWI anapojitokeza na hizo alama huwa ugonjwa ushafika mbali na yuko karibu na kikomo. Analinganisha na mchezo wa keramu tena kwani mchezaji anapotia kingi huwa anamalizia bao hilo au mwanamke anapovunja chupa wakati wa kujifungua huwa yuko tayari kumtoa mtoto.

Mtunzi katika ubeti wa 274 anauliza swali la balagha ambalo halihitaji jibu bali ni la kusisitiza tu.

Kwani kutaka arusi
Na mwano una virusi
Kama ni wewe ikisi
Hoyo ngalimpokeya (ub.274)

Swali hili lisilohitaji jibu analitumia kusuta wazazi wanaowaoza watoto wao hali wanajua kuwa wana UKIMWI na wanajua kuwa kama wanamume mwenye UKIMWI wangukuja kuwaposi binti zao hawangekubali kuwaoza.

Katika ubeti wa 277-278 mwandishi anaonyesha kuwa ugonjwa huu ni adhabu kutoka kwa Muumba au ni rada ya Mungu kwa madhambi ya binadamu.

Uzunifu na liwati
Na kula uhasharati
Tukiwa hatuyawati
Na zibati zitakuya

Kwa Mungu kuna zibati
Za mtu na za umati
Ukiadiya wakati
Zikali huwapijia (b.277-278)

Kuchapwa vibati au vikoto ni taswira ya adhabu ya Mungu. Vikoto hutumika katika madrassa kuwaadhibu wanafunzi wanaokosea. Hivyo, mtunzi amelinganisha vikoto, hivi na vile vya Mungu kwa wanaokosea. Adhabu hii inaweza kuwa ya mtu binafsi au ya jamii nzima.

Hitimisho

Mwandishi wa utenziwa *UKIMWI ni Zimwi* husika amefaulu sana kuupitisha ujumbe wake kwa kutumia tamathali za usemi na taswira. Mtunzi amefaulu kutumia lugha iliyojenga picha na kuchochea hisia za wasomaji. Picha hizi zimeundwa kwa matumizi ya tamathali za usemi hasa tashibihii na sitiari. Tamathali hizi zimeundwa kutokana na mambo wanayoyafahamu binadamu, kama vile chakula kama donasi na sambusa, mazingira ya baharini na uvuvi, ya minazi, dini, masuala ya wale watu walioasi wakaadhibiwa na Mwenyezi Mungu kama Firauni, Karuni, watu wa Adi, Thamudi na Lut na kadhalika. Hivyo, zinakuwa na athari kubwa zaidi kwa wasomaji na binadamu kwa jumla. Athari ya ugonjwa wa UKIMWI inajitokeza kwa uwazi na uhalisi zaidi kwani umefafanuliwa kwa kuhusishwa na mambo ya kawaida. Imeonekana kuwa mtunzi ambaye ni shekhe/mwalimu wa dini na pia Mswahili amechota malighafi yake ya kuundia tamathali za usemi na taswira kutokana na dini, mazingira ya bahari, mchezo wanaocheza na vyakula wanavyovifahamu wanadamu. Uumbaji wa tamathali hizi ni muhimu katika kukamilisha dhamira na maudhui ya utenzi huu.

Marejeleo

- Chiraghdin, S. (1973). *Utangulizi wa Sauti ya Dhiki*. Nairobi: Oxford University Press.
- Doctors of the World (2001-2006). *HIV/AIDS Strategic Plan*, Medecins du Monde-International.
- Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Oxford: Clarendon Press.
- Kunene, M. (1979). *Emperor Shaka the Great: A Zulu Epic*. London: Heinemann Educational Books Ltd.
- Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.
- Miller C. (1990). *Theories of Africans: Francophone Literature and Anthropology in Africa*. Chicago and London: University of Chicago Press.
- Ministry of Health (2001). *AIDS in Kenya* (6th Edition). Nairobi: Governemnt Printers.
- Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*. Nairobi. East African Educational Publishers.
- Mulokozi, M. M. (1989). 'Tanzu za Fasihi Simulizi'. Katika *Mulika* na. 21 Dar es-Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Uk. 1-24.

Mulokozi, M. M. na Kahigi K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar-es-Salaam. Tanzania Publishing House.

Wamitila, K. W. (2001). *Archetypal Criticism of Kiswahili Poetry*. Bayreuth: Africa Studies 57.

_____ (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus books.